East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Usawiri wa Vijana wa Kisasa katika Riwaya ya Dunia yao ya Kiswahili

*Dkt. Naomi Nzilani Musembi, PhD[1*] na Dkt. Fred Wanjala Simiyu, PhD[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Cha Jaramogi, S. L. P. 210 - 40601 Bondo – Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Kibabii, S. L. P. 1699-50200 Bungoma – Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: nmusembi@jooust.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*02 Januari 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Vijana, Usawiri, Riwaya Mpya.*

**IKISIRI**

Makala hii itachunguza usawiri wa vijana katika dunia ya sasa inayobadilika kila uchao. Itafanya hivi kupitia uchanganuzi wa riwaya mpya ya Dunia Yao (2006) ya S.A Mohamed. Utafiti unaonyesha kwamba vijana kote duniani sasa wana utamaduni wao ambao watafiti wanaueleza kama 'ulimwengu huru' wa vijana ulio na mitindo na njia za maisha ambazo, vijana hufuata ili kujitofautisha na utamaduni wa wazazi wao. Utamaduni wa vijana kwa kiasi kikubwa ni zao la maendeleo katika jamii za ulimwengu. Kadri jamii inavyosonga mbele kimaendeleo, ndivyo ambavyo utamaduni wa vijana unakuzwa, unaimarishwa na kusambazwa miongoni mwa vijana kote duniani. Vijana wamebuni utamaduni wao kama njia moja ya kuasi dhidi ya utamaduni uliotawaliwa na wazee. Wanataka kujihusisha na tabia kama matumizi ya dawa za kulevya, ushoga, uasi wa maadili ya kijamii, Mitindo mipya ya mavazi, muziki miongoni mwa tabia nyingine ambazo wanajua huwatenga wazee. Hii ni tabia ibuka ya vijana kupania kuonyesha nguvu na uwezo wao katika jamii. Ujumbe wanaopitisha ni kuwa hawako tayari kushiriki utamaduni unaowadhibiti na kuwanyima nafasi yao katika jamii. Malengo mahususi yatakayoongoza makala haya ni pamoja na kuangazia sifa za vijana wa kisasa na wakati huo huo kufafanua njia mabazo wanajamii wanaweza kutumia ili kujaribu kuziba mwanya mpana uliopo kati ya kizazi cha jana na cha leo. Makala hii itaongozwa na nadharia ya uhalisia. Mhimili mkuu wa nadharia ya uhalisia ambao utaongoza makala ni kwamba, fasihi ni kioo cha jamii na inapaswa kumulika maisha kama yalivyo. Muundo wa kimaelezo utatumika kuchanganua data. Data itakusanywa kutokana na kusoma riwaya teule na kudondoa sehemu zinazolingana na malengo ya utafiti. Data itadondolewa, itanukuliwa, itapangwa kisha kuchanganuliwa kulingana na mada husika.

**APA CITATION**

Musembi, N. N. & Simiyu, F. W. (2024). Usawiri wa Vijana wa Kisasa katika Riwaya ya Dunia yao ya Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 1-10. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669.

**CHICAGO CITATION**

Musembi, Naomi Nzilani and Fred Wanjala Simiyu. 2024. "Usawiri wa Vijana wa Kisasa katika Riwaya ya Dunia yao ya Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 1-10. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

**HARVARD CITATION**

Musembi, N. N. & Simiyu, F. W. (2024) "Usawiri wa Vijana wa Kisasa katika Riwaya ya Dunia yao ya Kiswahili", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 1-10. doi: 10.37284/jammk.7.1.1669.

**IEEE CITATION**

N. N. Musembi, & F. W. Simiyu "Usawiri wa Vijana wa Kisasa katika Riwaya ya Dunia yao ya Kiswahili", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 1-10, Jan. 2024.

**MLA CITATION**

Musembi, Naomi Nzilani & Fred Wanjala Simiyu. "Usawiri wa Vijana wa Kisasa katika Riwaya ya Dunia yao ya Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Jan. 2023, pp. 1-10, doi:10.37284/jammk.7.1.1669.

## UTANGULIZI

Mabadiliko makubwa katika tabia na mienendo ya vijana wa kisasa yanahusiswa pakubwa na vijana ambao hushiriki misingi sawa kote duniani (Kaplan, 1989, Brake, 1980). Brake anaeleza kuwa mienendo ya vijana husimilishwa, hufikiwa na kusambazwa kupitia teknohama. Njia za teknohama kama huduma za mtandao, setilaiti, runinga, na simu janja hutumika kuzalisha tamaduni mpya za vijana zinazojikita katika muziki, filamu, mavazi, na mitindo ya maisha pamoja na bidhaa wanazotumia. Kuanzia Karne ya ishirini, suala la mabadiliko ya vijana limeangaliwa kama mabadiliko yanayotokana na mchanganyiko wa mawazo, na migogoro katika kuchanganya utamaduni na maendeleo. Tofauti za kimaadili zinajitokeza wakati taasisi za kijamii zinaposhindwa kumshikilia mwanajamii na kumwacha aingie katika dunia mpya yenye utamaduni tofauti. Vijana katika riwaya ya *Dunia Yao* wamesawiriwa kuwa waasi. Vijana wanatenda vitendo kwa hiari na wamekengeuka na kuathiriwa na tamaduni mbalimbali wanazokumbana nazo kupitia mitandao mbalimbali. Kuathiriwa huku huzua maarifa, ubunifu na upenyefu wa fikra miongoni mwao. Mwandishi Said Ahmed Mohamed ameyasawiri mabadiliko ya vijana huku akitomelea wazo kwamba, mabadiliko yanayosababishwa na upenyefu huu wa fikra miongoni mwa vijana huwapelekea baadhi ya wanajamii kuwaona vijana kama waasi wa maadili ya jamii.

Mwandishi S.A Mohammed (*Dunia Yao*, 2006), anaonekana kutumia taswira ya vijana wa kisasa kama mkakati wa kuibua falsafa yake kuhusiana na suala nzima la mabadiliko na mienendo hasi ya vijana. Kupitia riwaya hii, anawamulikia vijana masaibu yanayowakumba, chanzo cha masaibu hayo, na wakati huohuo, kuwaonyesha njia ambazo wanaweza kutumia ili kujinasua kutoka kwa masaibu hayo.

Siku hizi, kutokana na mabadiliko ya maisha na kukengeuka kwa wanajamii kutokana na utamaduni wa kimagharibi, vijana huasi utamaduni wao na hutenda vitendo kwa hiari. Hii ni kutokana na athari wanayopata kutokana na kukengeushwa na kuathiriwa na tamaduni mbalimbali wanazokumbana nazo kupitia mitandao mbalimbali. Kuathiriwa huku huzua maarifa, ubunifu na upenyefu wa fikra miongoni mwa vijana (Wamitila, 2008; Kaui, 2008; Musembi, 2018; Musembi, 2022). Mabadiliko yanayosababishwa na upenyefu huu wa fikra miongoni mwa vijana huwapelekea baadhi ya wanajamii kuwaona vijana kama waasi wa maadili ya jamii. Hatima yao ni kuonekana kama waasi wanaotenda yasiyosadifu na hivyo kupelekea mitafaruku kati yao na wanajamii kwa jumla. Mwandishi wa riwaya ya *Dunia yao* S.A. Mohamed amesawiri vijana wa sasa katika dunia yao akiwa na nia ya kuonyesha sababu ya mwanya mkubwa uliopo katika dunia ya jana na dunia ya sasa miongoni mwa vijana na wazee. Kwa kufanya hivyo, mwandishi anamwachia msomaji wake wajibu wa kuamua njia mwafaka inayoweza kutumiwa na wanajamii ili kuleta mwafaka kati ya kizazi cha jana na cha leo katika ulimwengu huu unaobadilika.

## USAWIRI WA VIJANA KATIKA RIWAYA YA *DUNIA YAO*

*Dunia Yao* ni riwaya mpya ya Kiswahili ambayo inawasawiri vijana katika Dunia yao. Vijana, kulingana na mwandishi wa riwaya hii wana sifa ambazo ni tofauti na za jamii yao. Wanaonyesha kukengeuka kutokana na utamaduni wao wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

Kiafrika na kupapia utamaduni wa kimagharibi. Aidha, vijana wanakumbwa na matatizo mengi ambayo yanawapelekea kutenda vitendo ambavyo wazee wanaviona kuwa ni uasi na okosefu wa heshima. Uasi huu unaonyeshwa kupitia njia zifuatazo:

**Ni Waasi wa Mila na Utamaduni Wao**

Kwa sababu ya mabadiliko ya maisha yanayosababishwa na usasa, vijana katika jamii ya sasa wamekengeuka kutokana na mila na utamaduni wa wazazi wao. Vijana wamebuni utamaduni wao kama njia moja ya kuasi dhidi ya utamaduni uliotawaliwa na wazee. Hawako radhi kufungwa katika silisili za utamaduni unaowakandamiza kama anavyosema Yungi kupitia Uk. (25):

> *"Lazima…uukubali ukweli. Wakati umebadilika. Watoto kuanzia sasa watawaendesha wazee wao. Pia huu ni wakati wa wanawake kuwakimu na kuwaongoza wanaume… Hakuna cha mila wala desturi. Hakuna mswalie mtume wala mswalie nini…".*

Vijana kote duniani sasa wana utamaduni wao ambao Brake (1980) anaueleza kama 'ulimwengu huru' wa vijana ulio na mitindo na njia za maisha ambazo, vijana hufuata ili kujitofautisha na utamaduni wa wazazi wao. Utamaduni wa vijana kwa kiasi kikubwa ni zao la maendeleo katika jamii za ulimwengu. Maadamu kadri jamii inavyosonga mbele kimaendeleo, ndivyo ambavyo utamaduni wa vijana unakuzwa, unaimarishwa na kusambazwa miongoni mwa vijana kote duniani. Vijana wanataka kujihusisha na tabia kama matumizi ya dawa za kulevya, ushoga, uasi wa maadili ya kijamii, mitindo mipya ya mavazi, muziki mpya miongoni mwa tabia nyingine ambazo wanajua huwatenga wazee.

Mwandishi anamulika uasi huu wa mila na itikadi za kijamii kupitia kwa wahusika kama Bori. Bori amekengeuka kabisa kutoka kwa utamaduni wa jamii yake. Mavazi yake yanaonyesha uasi. Miondoko yake anapotembea pia yanatangaza uasi wa mitindo iliyozoeleka na jamii yake. Ndi anasema miondoko ya vijana ni ya ajabu. Ni miondoko ambayo wazee hawajapata kuiona maishani mwao (Uk. 32). Dubwa pia ni muasi. Amelelewa katika familia ya Kiislamu lakini amebadilisha dini akawa mkristo. Kulingana na babake Ndi, Dubwa anaonyesha kuchanganyikiwa na hana msimamo wowote maishani. Yungi pia ni muasi wa utamaduni uliomzaa na kumlea. Msichana katika utamaduni wa mwafrika na hasa aliyezaliwa katika dini ya Kiislamu anapashwa kuwa bikira mpaka atakapoolewa. Hapaswi kuonekana akitembea na wanaume kabla ya kuolewa. Yungi kulingana na babake ni kahaba na chakula anacholeta nyumbani ni cha ukahaba suala ambalo linampelekea babake kukisusia chakula hicho.

Vilevile, tabia ya Yungi ya kulewa na kufika nyumbani usiku ni uasi. Mwanamke wa Kiafrika kulingana na Kimilu (1962) hatarajiwi na jamii kushiriki vileo kutokana na majukumu ambayo jamii imemtwika. Aidha, kwa mujibu wa utamaduni wa Kiafrika, msichana hapaswi kuleta wanaume na kulala nao nyumbani kwa wazazi wake kama anavyofanya Yungi.

Kulingana na Kaplan (1989), uasi wa vijana wa mila na utamaduni wao ni jaribio lao la kupania kuonyesha nguvu na uwezo wao wa kijamii. Ujumbe wanaopitisha ni kuwa hawako tayari kushiriki utamaduni unaowadhibiti na kuwanyima nafasi yao katika jamii. Ni kutokana na uasi huu ambapo Yungi anamkosea mamake Bi. M heshima kwa kumwambia kwamba yeye mamake amezeeka na amepitwa na wakati (Uk.113).

Kuacha mila na utamaduni kwa vijana ni jambo ambalo wazee wanalikashifu. Japo wanajua fika kwamba wakati umefika wa vijana kuonyesha nguvu zao katika kuleta mabadiliko katika jamii, wazee wanashikilia kwamba kuacha mila na utamaduni kabisa kwa vijana ni kupotoka kabisa. Ndi anawashauri vijana kushikilia utamaduni wao kwa kuwapigia methali kupitia (Uk. 192). Anasema:

> *" Shindaneni nao lakini mjue ng'ombe anayewachiliwa huru kutoka zizini kwao, lazima ahifadhi njia ya kurudi kwao".*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

Huu ni ushauri mwafaka kutoka kwa mwandishi wa riwaya ya *Dunia Yao* kuhusu vijana kwamba, ni muhimu vijana wajifunze kuishi vizuri na wazazi na walezi wao kiasi kwamba, hata wakitoka nyumbani kutokana na harakati za kutafuta kazi, wakumbuke utamaduni wao bila kuasi. Hii ndio falsafa ya mwandishi S.A Mohamed kuhusiana na umuhimu wa vijana kuifadhi utamaduni wao.

Mwandishi anaelekea kutoa suluhu la ukata tamaa miongoni mwa vijana kwamba, iwapo vijana watapata kazi, hasa nchini mwao, baadhi ya tabia hasi wanazohusishwa nazo vijana zitapungua.

**Vijana Wamekata Tamaa**

Ukata tamaa ni hali inayosababishwa na kutotimia kwa malengo fulani. Mtu anapokata tamaa huonyesha dalili ya kutojali jambo lolote liwe zuri au baya. Dollard (1939) akinukuliwa na Kavuria (2008) anaeleza kuwa mtu huweza kukumbwa na hali ngumu ya maisha na ashindwapo kuisuluhisha huweza kukumbwa na hali ya kukata tamaa. Viwango vya ukataji tamaa miongoni mwa vijana katika jamii ya leo vimeongezeka kutokana na ukosefu wa kazi, hali ngumu ya maisha, kufiwa na wazazi, unyanyasaji wa kimapenzi, miongoni mwa hali nyingine nyingi. Kutokana na ukataji tamaa, baadhi ya vijana hujitia kitanzi, wengine wanaungua ugonjwa wa akili, wengi wanaanza tabia hasi kama kutumia mihadarati na kushiriki vileo. Aidha, wengine wanajitosa katika ufuska ili kujikimu bila kusahau wale ambao wanakuwa majangili na kuanza wizi na ubakaji.

Mwandishi wa riwaya ya *Dunia yao* amesawiri hali hii kwa weledi mno. Anonyesha taswira ya vijana ambao wamekata tamaa na kuanza vitendo vya ushari. Viwango vya ukata tamaa miongoni mwa vijana vimemulikwa kupitia wahusika kama Yungi, Mtima, Jitu, Bori, na Dubwa. Yungi ni msichana ambaye kutokana na hali nyumbani kwao, anajitupa katika maisha ya ufuska ili aweze kuikimu familia yake. Babake ambaye anapaswa kuikimu familia amejiambaa nayo. Hanunui chakula na wala hatangamani na watoto na bibi yake. Yungi anachukua jukumu la kushiriki umalaya ili aikimu familia yake. Tunaambiwa anafanya hivi kwa kukata tamaa kwani hakuna mwingine wa kuchukua jukumu hilo ila yeye. Hili linatokana na babake Ndi kuitelekeza familia yake na kujifungia katika ulimwengu wake mdogo. Mtima naye kutokana na hali tete nyumbani anaamua kuenda Uingereza kubadilisha maisha yake. Huko anapata maisha ni magumu mno na inabidi ajikakamue ili aweze kujikimu. Hali hii inampelekea kukata tamaa ya maisha mazuri. Anasema:

> *"Nimo tu mpaka sasa nagaragara kwa wenzangu ambao kwa muda mfupi wameshanichoka. Sina budi lakini kung'ang'ania. Ndiyo maisha ya huku yalivyo. Kila mtu hubeba mzigo wake. Kila mtu hujitaka mwenyewe… Baadaye nitakusimulia yote… Si hadithi nzuri. Ni ujahili mtupu. Kupiga moyo konde na kuuza roho… Lakini nifanyeje? Kama mnavyosema nyinyi wazee; Duniani hakukaliki, akhera hakwendeki! Hata kwao mtu si kwao tena!.."* (uk 116)

Toni ya uchungu na ukata tamaa inatawala maelezo ya Mtima. Inaonyesha hali ambayo haipendi lakini inabidi avumilie kwani hana suluhu. Ukata tamaa miongoni mwa vijana inasababishwa na ukosefu wa kazi japo wamesoma. Mtima anapoondoka nyumbani kwao na kuelekea Uingereza anapatana na hali ngumu mno ya maisha ambayo inampelekea kukata tamaa na kujifananisha na mfu. Kupitia kwake Mtima anatueleza hali yake tete ifuatavyo:

> *"…Sielewi kwa nini sijafa kabisakabisa. Nimebakisha mzizi wa tamaa, walau mmoja. Natamani ingekuwa vingine... Najua ulinikatalia kuja hapa kutokana na hofu yako kwamba na mimi ningekuwa Yungi. Hofu ya kuona vijana hatuna jingine la kufanya katika nchi yetu ila ubalaa, uchungu wa kuona hata elimu yangu bure tu."* (Uk 117).

Kutokana na kutopata kazi na maisha kuwa magumu mno Uingereza, Mtima anapata ugonjwa wa kiakili na kuanza kumeza tembe za kumuondolea ugonjwa wa kiherehere.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

Sio Mtima peke yake ambaye anaonyesha kukata tamaa. Jitu amekata tamaa ya kuwa na maisha mema na kuanza tabia ya wizi. Anaiba na kuuza chochote kile nyumbani hasa chupi za dadake Yungi. Kupitia Uk. (134), tunapata tabia ya wizi wa Jitu kupitia kwa kakake Bori:

> *"… kufa habithi we! Nyumba nzima umeimaliza wewe. Nilikuonya ulipotaka kuhamisha vitu chumbani mwa mama na baba…" Naye Yungi dadake anailalamikia tabia ya kakake ya kuiba anaposema: "…Umeniibia mpaka chupi zangu…"* (Uk. 135).

Taswira anayotuchorea mwandishi ya familia ya Ndi ndiyo inayotuelekeza kufahamu kwa nini Jitu amekuwa mwizi, Yungi kahaba, Dubwa kuondoka nyumbani na Mtima kughura kuelekea Ughaibuni. Ndi ambaye ni babake amejitenga na familia yake. Ameshindwa kuikimu na kuidhibiti hivyo basi vijana hawana lingine ila kukata tamaa na kuanza kutenda vitendo visivyofaa. Hapa lawama inaonekana kuelekezwa na mwandishi kwa Ndi ambaye ni baba wa watoto hawa ambao ameshindwa kuwakimu na kuwadhibiti. Badala yake anajitenga nao na kujifungia katika ulimwengu wake pasi na kujali hatima ya watoto na mkewe.

### Vijana Kutoka Bara Afrika Wanateseka Ughaibuni

Ukosefu wa kazi kwa vijana kutoka bara Afrika limekuwa donda sugu katika jamii ya kisasa. Vijana wanapokata tamaa ya kupata kazi kwao, wanaamua kugura ughaibuni ili kutafuta kazi wakiwa na matumaini ya kubadilisha maisha yao. Lakini hali inawawia vigumu huko ughaibuni. Wanapata mateso si haba huko kutokana na ubaguzi wa rangi na wa asili. Wengi wao wanaishia kujitia kitanzi ama miili yao inakuwa chakula cha marisasi. Hali hii tata ya vijana wenye asili ya Kiafrika wakiwa ughaibuni tunaichorewa vyema na mwandishi kupitia kinywa cha Mtima. Mtima anapofika Uingereza, hali inakuwa si hali tena. Matarajio yake ya kupata kazi na kuwa tofauti na ndugu zake kifedha inasambaratika. Anaanza majuto kama anavyotusawiria mwandishi kupitia Uk. (116). Mtima anasema:

> *"…Natamani ningebaki nyumbani ingawa najua utaniuliza nyumbani ndiko wapi. Ningalitamani unganikatalia kuja huku ingawa najua nisingekubali… ingekuwa jambo bora kwangu kama wewe na mama mnepinga kuondoka kwangu. Mgenizuia. Ningekuwa na nafasi yangu tu kujilaumu…Makundi kwa makundi tuko mabarazani tunazembea…"*

Majuto ya Mtima yanatokana na kubaghuliwa kikazi Uingereza. Hapati kazi kwani nafasi za kazi zinachukuliwa na wageni wenye rangi nyeupe waliojaa nchini (Uk. 117). Ubaguzi anaofanyiwa Mtima Uingereza unatokana naye kutokuwa wa asili ya Kitaliano, Kiarabu, na Kiingereza. Mtima anateseka mbali na kwao, Kupitia uk. (117), anasema:

> *Sina budi kuboboja kukata tamaa kwangu. Maisha yameshanipa mgongo. Ni hadithi isiyo mashiko, isiyo maana… wewe wajua mtu anapofikia ukomo huu. Anapoganda…"*

Hali hii inampelekea Mtima kupata ugonjwa wa kiakili ambao unamlazimu kumeza vidonge vya usingizi kupoza ugonjwa wa kiherehere uliompata kutokana na hali yake ya mateso. Hali hii anaileza vizuri Mtima kwa kusema:

> *… Kwa hivyo naandika haya machache kabla sijala vidonge vya usingizi walivyonipa kupoza kiherehere change… Mwezi wa sita sasa, wamegundua naumwa na kiherehere ambacho wao wanakiita 'depression'* (Uk 118)

Kuteseka kwa Mtima Uingereza si hali ngeni kwa msomaji. Vijana wa sasa hata wakienda Ughaibuni na wapate kazi huwa ni kazi ngumu na zisizo na heshima yoyote. Wanafanya kazi za sulubu kama watumwa. Malipo mkia wa mbuzi kama ayaitavyo Mtima Uk. (120). Aidha, huwa hawana bima, hawana ulinzi pia. Taswira hii ya mateso ya vijana ughaibuni inazua falsafa ya mwandishi wa riwaya ya *Dunia Yao* kwamba,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

badala ya vijana kutafuta kazi ughaibuni kunako mateso na ubaguzi wa rangi, itakuwa mwafaka kwao kukaa na kujitaftia riziki nyumbani kama anavyosema Mtima, kinywa cha mwandishi kupitia nukuu hili 'afadhali kufia ujuako kuliko usikojua" (Uk.117). Mwandishi anaelekea kutoa suluhu la ukata tamaa miongoni mwa vijana kwamba, iwapo vijana watapata kazi, hasa nchini mwao, baadhi ya tabia hasi wanazohusishwa nazo vijana zitapungua.

**Ukosefu wa Nafasi za Kazi kwa Vijana**

Hata ingawa vijana wamesoma, hawapati kazi. Ukosefu wa kazi unawapelekea baadhi ya vijana kujihusisha na tabia hasi kama matumizi ya dawa za kulevya, ulevi, ukahaba, vitendo vya kuhuni kama ubakaji na wengine hukumbwa na ugonjwa ya kiakili maarufu kama *depression*. Mtima anaondoka kwao kuelekea Uingereza kutafuta kazi. Atokako hakuna kazi. Anatueleza hilo kupitia Uk. (117) anaposema:

> *"…Hofu ya kuona vijana hatuna jingine la kufanya katika nchi yetu…Uchungu wa kuona hata elimu yangu bure tu…"*

Hali hii inawapelekea vijana kuzembea na kushiriki katika tabia zisizofaa. Ndi anaeleza hali hii kupitia Uk. (32) anaposema:

> *"...Salama yake hatukumpata…tungemfirigishafirigisha hapahapa bila ya kumfikisha polisi wanakoachiwa…Vijana waliokuwemo kundini hapo walicheka na kukariri kila mara yes… yes… yes…"*

Hali hii inaonyesha vijana wa sasa kutokana na ukosefu wa kazi wanalowela tu mijini na kukaa ovyo kwa vikundi huku mara kwa mara wakishiriki katika vitendo vya kihuni. Kutokana na ukosefu wa kazi, na kutoshirikishwa kwa vijana katika maendeleo ya nchi, vijana wengi wanaishia kujitumbukiza katika wizi, umalaya, ulofa, matumizi ya dawa za kulevy,a na wengi kutokana na maovu haya, hupatwa na magonjwa ya zinaa kama ukimwi. Yungi amekuwa akimeza tembe ambazo hataki zikionekana.

Wakati mwingine kutokana na ukosefu wa kazi vijana wanajipata wakitumia mihadarati na kuwaibia watu. Hali hii imemulikwa vyema na mwandishi kupitia Uk. (32) anaposema:

> *"Angefanyaje na ile bastola bandia alidhani bastola ya kweli?... vijana wanatafuta pesa ya unga. Hawana kiwewe wala kisisi tena. Hawaogopi kamwe… mchana wote huu; kweupeeee".*

Sio wizi na kutumia mihadarati tu lakini pia ukosefu wa kazi unawapelekea vijana kukumbwa na ugonjwa wa akili kutokana na ukata tamaa. Ugonjwa huo wa akili huwaondolea waathiriwa hata usingizi mpaka wameze vidoge vya usingizi. Mtima ni majeruhi wa ugonjwa wa akili kutokana na hali ngumu aliyokumbana nayo Uingereza. Anamweleza babake hali hii kwa kusema:

> *"Maisha yameshanipa mgongo. ... Lazima nizungumze na nafsi yangu. Ni njia pekee iliyobaki ya kutomalizika kabisakabisa. Wewe unajua mtu anapofikia ukomo huu. Anapoganda. Kwa hivyo, naandika haya machache kabla sijala vidonge vya usingizi walivyonipa kuponza kiherehere changu… mwezi wa sita sasa, wamegundua naumwa na kiherehere ambacho wao wanakiita depression…" (Uk. 118).*

Ni kutokana na ukosefu wa kazi ambapo Yungi naye amejitosa katika umalaya ili ajikimu na aikimu familia yake.

Si Barani Afrika tu ambapo kazi ni nadra. Hata Ughaibuni kazi hazipatikani na chache zilizopo hugang'aniwa na kila mtu. Mtima anasawiri taswira hii kupitia Uk. (123) anaposema:

> *" Nilianza kutafuta kazi. Kwa muda wa miezi minane sikupata kazi yoyote na kwa muda wa miaka minne sasa , sina kazi ila ya kufagia na kufuta mavumbi dukani. Kazi zilizopo ni chache na zinagombaniwa na kila mtu, wakiwemo Warusi, na jamaa wa Ulaya ya Mashariki"* (Uk. 123).

Taswira hii si ngeni hapa nchini Kenya ambapo vijana japo wamesoma na kupata shahada katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

Nyanja mbalimbali wanajipata wakifanya kazi duni sana maarufu kama "kazi mitaani" na malipo yake ni duni sana. Wasichana nao hujipata wakifanya kazi duni sana hususan kuosha vyombo, kutandika vitanda hotelini, kupiga pasi miongoni mwa kazi nyingine duni. Mtima anaisawiri hali hii vyema katika Uk. (123). Ukosefu wa kazi miongonim mwa vijana waliosoma na kuhitimu vyema vyuoni unawapelekea vijana kukata tamaa ya kuendelea na masomo kama anavyosema Mtima:

> *" Nilijaribu kwenda kujiendeleza kielimu. Nilitaka kupata degree ya sayansi ya kompyuta. Mimi nilitaka lakini moyo ulikataa. Niliona adha kusoma. Kuna kitu kilichoniambia kwamba elimu haina maana. Haikunifaa hapa. Ya nini basi*? (Uk.124).

Huu ni ukata tamaa na utafiti umeonyesha kwamba vijana wengi huambulia hali ya kukumbwa na adha na ugonjwa wa kiherehere maarufu kama *depression* kutokana na hali ya kukata tamaa.

Suala la ukosefu wa kazi na athari zake hapa nchini Kenya limekuwa sugu mno japo vijana wengi wamesoma. Vijana wanajipata wakilowela mijini wakitafuta kazi na zikikosekana baadhi yao wanajiingiza katika vitendo hasi ili kujikimu. Hili ndilo mwandishi wa riwaya ya Dunia Yao amelimulika ili suluhu iweze kupatikana na kubadilisha maisha ya vijana waliokata tamaa katika dunia yao. Mwandishi anaelekea kutoa suluhu la ukata tamaa miongoni mwa vijana kwamba, iwapo vijana watapata kazi, hasa nchini mwao, baadhi ya tabia hasi wanazohusishwa nazo vijana zitapungua. Mwandishi anaelekea kuzindua vijana wa kisasa kwamba, kugura na kuelekea ughaibuni kutafuta kazi kuna matatizo yake kama yaliyompata Mtima. Ni heri kujiajiri na kupata kidogo chenye heshima pasi na udunishwaji wa aina yoyote.

**Vijana ni Weledi katika Teknolojia ya Kisasa**

Hii ni kutokana na athari wanayopata kutokana na kukengeushwa na kuathiriwa na tamaduni mbalimbali wanazokumbana nazo kupitia mitandao mbalimbali. Kuathiriwa huku huzua maarifa, ubunifu, na upenyefu wa fikra miongoni mwa vijana. Mtima alipofika Ugaibuni, anamnunulia babake kompyuta kama zawadi kwani alijua fika kwamba kompyuta hiyo itakuwa mwenzake babake kutokana na hali ya upweke aliyokuwa akiishi (Uk. 7). Vilevile, Mtima alijua babake atahiitaji katika mawasiliano yao kuliko matumizi ya barua. Mtima anasema:

> *" Utakapokwisha kujifunza kuitumia tutakuwa karibu sana kuzungumza. Kupitia baruapepe bila shaka … Bado sijapata pahala maalum pa kuishi. Kwa hivyo sina anwani ya kukupa.Lakini anwani ya posta ya nini siku hizi? Huu ni ulimwengu wa kompyuta"* (Uk.7).

Mtima alimnunulia babake kompyuta kutoka kwa posho lake la kwanza. Posho la pili anasema atajinunulia kompyuta yake ili aweze kuwasiliana kila mara na babake (Uk. 7). Hii ni ithibati tosha kwamba vijana wa sasa wakiwakilishwa na Mtima wanatiia maanani sana matumizi ya matadao katika kurahisisha mawasilianao. Mtima anapuuza matumizi ya awali ya barua anapomwambia babake "Lakini anwani ya posta ya nini siku hizi? Huu ni ulimwengu wa kompyuta" (Uk. 7).

Aidha, Bori japo alishindwa kuingia darasa la kumi na moja, na kutoweza kuendelea na masomo, anaonyesha kupenda teknolojia ya kisasa. Bori alipenda kuokota vyombo vya umeme na kuviunganisha. Babake Ndi anasema kutokana na tabia ya Bori ya kacharakachara huku akiokota chochote kile kinachohusu umeme, siku moja kulizuka miripuko ya moto ndani ya nyumba yao iliyosababishwa na utundu wa Bori wa kuchezea na kutaka kupatanisha vitu visivyopatana (Uk. 111). Bori aliuunganisha stima lakini siku moja ikamkausha kama tunavyoambiwa na Ndi kupitia Uk. (152):

> *"… Baadaye ndipo nilipokuja kujua kwamba Bori alichukuliwa na umeme aliokuwa akiuchezea. Bori akawa mhanga wa teknolojia ya kisasa aliyoipenda pasi na kuijua."*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

Aidha, vijana wamesawiriwa kuwa wapenda utandawazi. Ndi anaeleza hali hii katika Uk. (192) anaposema:

> *"…Mnakuja wakati ndani mmeujaza usasa na utandawazi tu. Mnaona upuzi asili yenu".*

Vijana wa Leo ni Huru

Mwandishi amewasawiri vijana kama viumbe huru ambao wanajiamulia hatima yao bila kuwahusisha wazazi wao. Wanaishi katika 'ulimwengu huru' ambao una mitindo tofauti naya wazazi wao. Mtima anaamua kugura na kuelekea Uingereza pasi na kuwahusisha wazazi wake Katika Uk. (116), Mtima anasema:

> *… Ungalinikataza kuja huku ingawa najua nisingekubali. Ningeng'ang'ania!"*

Maneno ya Mtima yanaonyesha vijana wana uhuru wao wa kujiamulia watakalo na hata wazazi wao wakijaribu kuingilia wanakaidi ushauri wao. Babake hajui ni lini Mtima alipata vyeti vya kuwezesha usafiri wake.

Aidha, Yungi naye anamzomea mamake kwa kung'ang'ania kuwadhibiti watoto wake pasi na kuwapa uhuru wa kutenda mambo wapendavyo. Yungi anamwambia mamake:

> *" Fungua macho… majirani wote wanawaachia watoto wao wa kike na wa kiume wafanye wanavyopenda siku hizi. Wewe bado unang'ang'ania ukale. Wewe bado unataka kukamata na kudhibiti. Unataka uongozi usiouweza. Huwezi tena kutuendesha"* (Uk. 25).

Kauli ya Yungi inaonyesha wazi kwamba katika dunia ya vijana, wako huru na hawataki kudhibitiwa na wazazi wao. Hii ndiyo sababu iliyopelekea Dubwa kuhama nyumbani kwao bado akiwa mbichi na 1 kuanza kuishi kivyake mbali na wazazi wake ili awe huru (Uk 137)

Pia, baadhi ya vijana wakihitimu vyuoni hutaka kujitenga na wazazi wao na kuishi mbali nao ili mzigo wa kuwakimu wazazi na familia nzima usiwaegemee. Wanataka kuwa huru. Dubwa ni mfano mzuri. Alipohitimu chuoni alihama kwao. Babake Ndi anaeleza hali hii kupitia Uk. (137):

> *"Dubwa ndiye aliyewasha upupu wa ubinafsi kwanza. Alipomaliza masomo yake chuo kikuu, hakutaka tena kuishi nasi. Hakutaka kutuona tena…Nadhani baada ya kuona kule kuporomoka kwangu, alihisi tungemwelemea mno. Mzigo mkubwa kwake ungemwelemea…"*

Uhuru wanaotaka vijana wa kutaka kuishi mbali na wazazi wao baada ya kumaliza masomo vyuoni na kupata ajira si suala ngeni katika jamii ya msomaji. Wengi wa wazazi hujikakamua kuhakikisha watoto wamesoma, japo kwa kuuma meno lakini watoto hao huwatenga wazazi wasije wakawa mzigo kwao. Babake Dubwa anaeleza hali hii ya kutelekeza wazazi kupitia uk. (137):

> *"…Hakuutia mguu nyumbani kwetu, nasi nyumbani kwake. Tulikuwa na hisia hatutakiwi kwake… Nadhani alihisi tungemwelemea mno… Hakuwa na sababu wala lazima ya kutubeba kama tulivyombeba".*

Mwandishi hapa anachora taswira ya vijana katika jamii ya sasa ambao kwao, kuwakimu wazazi ni mzigo. Ili kujiepusha na kuubeba, wanaihari kuhama nyumbani na kuishi katika dunia huru bila kuwajali. Uhuru aliotaka Dubwa ulimpelekea kukengeuka kabisa na mazingira aliyolelewa. Akabadilisha mtindo wa mavazi (Uk. 140), na pia akabadilisha dini na kuwa mfuasi wa dini ya Kikristo. Babake Ndi anaieleza hali hii anaposema:

> *"… Juzijuzi tu alijiunga na madhehebu ya kuhubiri maangamizo na kuabudu giza makaburini. Miaka miwili iliyopita, naskia kaokoka… Juzijuzi alirejea Makka kuhiji. Si hasha, kesho utamkuta anaonja kinibu cha pombe"* Uk 140

Vilevile, mitindo ya vijana ya mavazi ambayo ni tofauti kabisa na ya wazee inaonyesha ari ya vijana kuwa huru kutenda walitakalo bila kufungwa na mila na tamaduni za wazee.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

Vijana wa sasa wana mitindo tofauti ya mavazi na miondoko mipya wanapotembea. Ndi anashuhudia mabadiliko haya ya mitindo ya vijana kupitia mavasi na miondoko na kusema hivi:

> *"Vijana waliokuwemo kundini hapo walicheka na kukariri kila mara yes…yes…yes…huku wakikata miondoko ya ajabu, miondoko ambayo wazee hawajapata kuiona maishani mwao. Miondoko iliyotiwa nakshi na zile suruali walizovaa zilizotiwa mharisho*" (Uk. 33).

Bori pia ana tabia za kuvalia kihuni kulingana na babake. Katika Uk. (111) Ndi, babake Bori anasema:

> *"Bori naye alikuwa na namna yake ya kususia mambo. Alikuwa akipenda kuvaa mayatu ya buti mabovu aliyoyaokota na alipokuwa akienda, alitwanga hatua kwa nguvu na kudunda hayo mabuti ardhini au sakafuni, hasa mbele za watu… Hapo aliposimama sasa, alikuwa kavaa suruali ya ajabu. Mguu mmoja ulikuwa mweusi na mwingine mweupe na mabuti makubwa ya kijeshi… Nywele zake za ki-Bob Marley, timtim, na ndevu…kama mimea iliyoota juu ya ardhi, Mwilini kajitupia kabuti lililopoteza rangi..mrudiko wa Vidani vya aina mbalimbali kifuani…Tumboni alikuwa na tattoo ya mkasi wa umeme wa kukatia miti…"*

Mabadiliko katika mtindo wa mavasi na miondoko kwa vijana wa sasa si jambo geni hapa nchini Kenya. Ni mtindo unaowatofautisha vijana na wazee na ambao unawaudhi baadhiya wazee kama anavyosema Ndi kupitia Uk. (33):

> *"…Ndiyo, wazee wengine waliudhika , lakini hakuna aliyedadisi wala kulaumu chanzo na sababu ya mambo haya ambayo siku hizi yamekuwa mtindo… Si ya kupita tu.*

Mitindo ya vijana katika riwaya ya Dunia Yao haidhihiriki katika mavazi na miondoko tu bali pia katika mitindi mipya ya kimaisha wanayoikopa kupitia utamaduni wa kimagharibi. Vijana wamejitosa katika mitindo aina ya fensi au carnival. Ndani ya fensi hiyo watu huvaa nguo za miujiza. Nguo za kujibadilisha na kujificha. Wanacheza kwa tafrija katika tamasha kubwa. Huu ni mtindi mpya wa kimagharibi. Hapa nchini Kenya vijana wanauita *Halloween* na wanashiriki katika sherehe hizo mwezi wa tano kwa kuvalia maleba ya aina tofauti tofauti. Nilipochunguza maana ya sherehe za *Halloween* niligundua kwamba vijana huzishiriki kwa nia ya "kuiga shetani". Huu ni mtindo wa vijana wa kisasa katika dunia yao. Haya ni maelezo yangu tu kuhusiana na Haloween

**Vijana Wamekosa Heshima kwa Wazee**

Baadhi ya vijana wameonyesha utovu wa nidhamu na heshima kwa wazee kupitia matamshi na miondoko yao. Yungi anawakosea wazazi wake heshima. Haonyeshi heshima kama inavyodhihirika kupitia Uk. (24). Tunaambiwa:

> *" Yapata saa tisa na nusu za alfajiri aliporudi, jimbi la kwanza lilipolia. Aligonga mlango, huku akikiendeleza kicheko alichokuja nacho. Lile kundi lake la suhuba lilikuwa limeshatoweka na gari".*

Tabia hii ya Yungi inaonyesha kwamba uso wake huna haya kwa wazazi wake anaokuja kubishia mlango usiku akitokakwa sherehe zake. Sio hilo tu lakini Yungi anamtupia mamake maneno makali na kusema :

> *"… kama miaka yote hii umeshindwa kumzuia bwana huyu kuwa mwamba katika nyumba hii…"* (Uk, 27).

Vilevile, ukosefu wa heshima wa Yungi kwa babake unatomelewa katika Uk. (76) anaposema:

> *" Potelea pote! Na asile mwana wa kutokula! Hata punji moja asile!*

Hapa Yungi amamrejelea babake ambaye alikuwa amesusia chakula cha ukahaba kama alivyokiita yeye kutokana na sababu kwamba kinanunuliwa na Yungi akitumia pesa anazopata kupitia ukahaba. Yungi vilevile haonyeshi heshima yoyote kwa wazazi wake kwani anawaleta

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1669

wanaume katika chumba chake cha kulala bila kujali kuonekana na yeyote yule.

**HITIMISHO**

Kupitia taswira mbalimbali zinazoibuliwa na mwandishi S. A. Mohamed katika riwaya ya *Dunia Yao*, kilio cha vijana kwa jamii zao kinasikika wazi.. Mosi, vijana wanatoa kilio kwa serikali yao kwamba, kutokana na ukosefu wa kazi, vijana wanaamua kughura nchi zao kutafuta kazi Ughaibuni ambako wanatumikishwa na kulipwa malipo duni. Hali hii inawapelekea wengi wao kupata hata magonjwa ya kiakili maarufu kama depression. Aidha, kutokana na ukosefu wa kazi, vijana wengi wameishia kutumia dawa za kulevya pamoja na vileo ili kujisahaulisha makali ya maisha. Pili, vijana wanatoa kilio kwa wazazi wao. Kwamba wazazi wanapaswa kuwajibika katika malezi na elimu ya watoto wao. Kutepetea kwa wazazi katika malezi huchangia vijana kuwa na mienendo hasi hususan umalaya na wizi. Hali hii ilijitokeza kupitia maelezo ya wazazi wa Mtima, Yungi na n.k kutelekezwa na baba mzazi kwa sababu yeye hujifungia tu. Hafuatilii mienendo ya watoto wake. Watoto nao kwa kukosa malezi wamebadilika wakawa malaya na wezi. Utepetevu huu kutoka kwa serikali na wazazi huchangia vijana kuonekana kuwa waasi. Taswira alizotuchorea mwandishi S.A. Mohamed za vijana kupitia riwaya ya *Dunia Yao zinaonyesha uhalisia wa maisha. Nadharia iliyoongoza makala inasisitiza kuwa, fasihi ni kioo cha maisha. Taswira ya vijana wa kisasa katika riwaya ya Dunia yao ni uhalisia wa vijana katika jamii yetu. Mwandishi anatumia taswira ya vijana kama* mkakati wake wa kuibua falsafa yake kwamba, vijana ni kundi muhimu katika jamii ya sasa na wanapotoa kilio chao kupitia mienendo inayoonekana kuwa hasi, kilio chao kinapaswa kusikilizwa. Aidha, mwandishi anakariri kwamba, vijana wa leo hawako radhi kushiriki utamaduni unaowadhibiti na kuwanyima nafasi yao katika jamii. Welewa huu utapunguza mikwaruzano iliyopo baina ya kizazi cha jana na kizazi cha leo. Aidha, huenda ukapunguza mwanya uliopo baina ya kizazi cha jana na kizazi cha leo.

**MAREJELEO**


Brake, M. ( 1980). *The Society of Youth Culture and Youth Subcultures: Sex,Drugs and Rock 'n' Roll?* London: Routledge and Kegan Paul.

Kaplan, E. A. (1989). *Rocking Around the Clock: Music,Television, Postmodernism and Consumer Culture*. London: Mathuen.

Kaui, M. (2008). *Usawiri wa Vijana katika Tamthilia teule za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta* (Haijachapishwa).

Kavuria, P. (2008). *Dhuluma Dhidi ya Watoto katika Riwaya Ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta* (Haijachapishwa).

Kimilu, D. ( 1962). Mukamba wa Wuo. Nairobi: East Africa Literature Bureau.

Mohamed, S.A. (2006). *Dunia Yao*. Oxford University Press: Nairobi, Kenya.

Musembi, N. N. (2018). Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii Inayobadilika, Karne ya 21. Tathmini ya Nyimbo za Jamii ya Wakamba. *Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la CHAUKIDU, SUZA.*

Musembi, N. N. (2022). Ukataji Tamaa Miongoni mwa Watoto katika Jamii ya Kisasa. Tathmini kutoka Riwaya ya Kiswahili. *Katika Jarida la CHAKAMA. Juzuu 1 uk. 141-147.*

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.